TOLEO MAALUM

# KINARA

## WA MAONO SEKTA YA AFYA

SEPT 04, 2026

Rais Mhe.

# Dkt. Samia

KINARA wa Mageuzi katika KupunguzaVifo vitokanavyo na uzazi kwa Mama na Mtoto Afrika.



Kutoka Hatari za Uzazi hadi Faraja: Safari ya Tanzania Ilivyopunguza Vifo vya Mama na Mtoto

# Hali Ilivyokuwa Kabla ya Maboresho katika Afya ya Mama na Mtoto

**Miaka kadhaa iliyopita Tanzania ilikuwa inakabiliwa na changamoto kubwa katika afya ya mama na mtoto.**

**1. Vifo vya Mama Wajawazito Vilikuwa Juu**
Zaidi ya wanawake 500 kati ya kila 100,000 waliokuwa wanajifungua walipoteza maisha, Sababu kubwa zilikuwa: Kupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua, Shinikizo la damu la ujauzito, Maambukizi, Kufika hospitalini kuchelewa.

**2. Wanawake Wengi Walijifungulia Nyumbani**
Wanawake wengi hasa vijijini walikuwa wanajifungulia nyumbani, Baadhi yao walisaidiwa na wakunga wa jadi bila vifaa vya kisasa. Dharura ilipotokea, hakukuwa na usafiri wa haraka kuwafikisha hospitalini, Hali hii iliongeza hatari kwa mama na mtoto.

**3. Upungufu wa Vituo na Wataalamu**
Ripoti za wizara zilionyesha: Baadhi ya zahanati hazikuwa na: Wauguzi wa kutosha, Dawa muhimu,Vifaa vya kujifungulia, Madaktari bingwa wa uzazi walikuwa wachache sana. Hospitali za wilaya hazikuwa na uwezo wa kushughulikia dharura zote.

**4. Vifo vya Watoto Wachanga**
Watoto wengi walifariki ndani ya siku 28 za kwanza baada ya kuzaliwa. Sababu zilikuwa: Kuzaliwa njiti, Uzito mdogo, Kukosa hewa wakati wa kuzaliwa Maambukizi, Hii ilikuwa hali ya kusikitisha kwa familia nyingi.



JIONGEZE
Tuwavushe Salama

# Safari ya Dkt. Samia Kuweka Msingi wa Uzazi Salama: Ilianza Kipindi akiwa Makamu wa Rais

**Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua kampeni ya kitaifa ya afya ya mama na mtoto iliyopewa jina la "Jiongeze Tuwavushe Salama".**

Akiwa Makamu wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua kampeni ya kitaifa ya afya ya mama na mtoto iliyopewa jina la ***"Jiongeze Tuwavushe Salama".*** Kampeni hii ililenga kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga, na kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa kila mama, hasa vijijini.

Dkt. Samia alisisitiza kuwa: Kila mama anastahili kujifungua salama hivyo kila kiongozi wa mkoa au wilaya awajibike kwa matokeo ya afya katika eneo lake Vifo vya mama si takwimu tu, ni maisha halisi yanayopotea kila siku. Tunapaswa kuchukua hatua sasa.

**Utekelezaji wa Kampeni ilijumuisha hatua zifuatazo:** Mikutano na wakuu wa mikoa na wilaya kufafanua wajibu wa kila kiongozi, Mafunzo ya wakunga na wauguzi wa vijiji ili kuongeza ufanisi na Mafunzo ya wakunga na wauguzi wa vijiji ili kuongeza ufanisi

Kampeni za elimu ya jamii kupitia redio, televisheni, na vikao vijijini
Mfumo wa kufuatilia maendeleo ya kila kituo cha afya (scorecards na ripoti za kila mwezi).

# Rais Dkt. Samia Alipoingia Ikulu Machi 19, 2021: Uzazi Salama Kutoka Kampeni hadi Vitendo Halisi na Matokeo zaidi



**Akaongeza Bajeti sekta ya afya, Eneo la uzazi na huduma za mama na mtoto alihakikisha kila wilaya inapata usaidizi wa kifedha na kiufundi Kutoka Wizara ya Afya.**

Mnamo mwaka 2021, baada ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alichukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa msukumo aliouanzisha akiwa Makamu wa Rais katika kampeni ya "Jiongeze Tuwavushe Salama" unakuwa matokeo halisi yanayoonekana kwa wananchi.

Akaweka Bajeti kubwa zaidi katika sekta ya afya, hususan uzazi na huduma za mama na mtoto, Alihakikisha kila wilaya ilipata usaidizi wa kifedha na kiufundi kutoka Wizara ya Afya.

Alihimiza uwajibikaji wa viongozi wa mikoa na wilaya: kila kifo cha mama kijaridiwe na kutoa taarifa alisema *"Hii si kampeni tena, ni maisha halisi yanayohitaji matendo, si maneno."*

*Hii ilisaidia kuondoa mzizi wa tatizo la ukosefu wa uwajibikaji uliokuwepo zamani, Kuongeza Huduma Karibu na Wananchi*

**KUPITIA MAAGIZO YAKE:**

Zahanati na vituo vya afya vilijengwa au kuboreshwa vijijini Hospitali za wilaya zikapatiwa vifaa vya kisasa vya uzazi, Ambulensi za dharura zilipelekwa katika maeneo yaliyo hatarishi zaidi

Madaktari wa uzazi na wauguzi waliajiriwa zaidi ili kuhakikisha hakuna mama anapoteza maisha kwa sababu ya ukosefu wa mhudumu

**Mfumo wa Rufaa na Dharura**, alisisitiza kuwa:
Kila kituo cha afya kiwe na mfumo wa rufaa wa dharura, Kila dharura ya uzazi iweze kushughulikiwa haraka, Teknolojia kama simu na data ya digital (DHIS2) zisaidie kufuatilia matukio

*Mfumo huu ulihakikisha kuwa mama yeyote aliye katika hatari angepelekwa hospitali inayofaa bila kuchelewa.*





## Dkt. Samia ndiye aliyeweka msingi wa mafanikio makubwa katika kupunguza vifo vya mama na mtoto Tanzania.

Kupitia uongozi wake wa vitendo uliowezesha matokeo ambapo Aligeuza kampeni ya *"Jiongeze Tuwavushe Salama"* kuwa sera halisi na Alionyesha kuwa **political will** ni kiini cha kuboresha huduma za afya

**1. Kuongeza uwekezaji katika afya ya mama na mtoto**

Katika kipindi chake, bajeti ya sekta ya afya imeongezwa kwa kipaumbele maalum kwa: Vifaa vya uzazi salama (delivery kits, damu salama, vifaa vya upasuaji), Dawa muhimu za wajawazito na watoto wachanga.
Hii imeboresha ubora na upatikanaji wa huduma vijijini na mijini.

**2. Upanuzi wa miundombinu ya afya**

Chini ya uongozi wake, kasi ya kukamilisha na kuimarisha: Vituo vya afya, Hospitali za wilaya, Vyumba vya upasuaji wa dharura (CEmONC), imeongezeka, jambo lililopunguza vifo vinavyotokana na kuchelewa kupata huduma.

KINARA
WA MAONO SEKTA YA AFYA



Swipe Left

**3. Kuimarisha huduma za afya ya msingi**

Serikali yake imeweka msisitizo mkubwa kwenye: Huduma za kliniki kwa wajawazito (ANC), Huduma za kujifungua chini ya wataalamu, Chanjo na ufuatiliaji wa watoto wachanga. Hili limeongeza idadi ya kina mama wanaojifungulia katika vituo vya afya badala ya nyumbani.

**4. Ushirikiano wa kimataifa na ufadhili**

Amefungua zaidi milango ya ushirikiano na taasisi za kimataifa, hatua iliyoongeza rasilimali kwa: Afya ya uzazi, Lishe ya mama na mtoto, Mafunzo kwa wahudumu wa afya.

**5. Uongozi wenye mwelekeo wa kijamii**

Akiwa mwanamke na kiongozi wa juu wa nchi, ameweka msisitizo wa kisera kwenye ustawi wa wanawake na watoto, jambo lililoongeza uhamasishaji na kipaumbele cha kitaifa katika suala hili.





KINARA
WA MAONO SEKTA YA AFYA
Swipe Left



## Matokeo chanya ya Safari ya Maboresho katika eneo la huduma za Afya ya Uzazi kwa wajawazito na watoto wachanga

**1 .Kupungua kwa vifo vya mama**
Kiwango cha vifo vya mama (Maternal Mortality Ratio) kimepungua kutoka takriban 556 kwa kila vizazi hai 100,000 (2015/16) hadi karibu 104 kwa kila 100,000 (2022) kulingana na ripoti za kitaifa za afya. Hii ni hatua kubwa kuelekea malengo ya maendeleo endelevu (SDGs).

**2. Kupungua kwa vifo vya watoto chini ya miaka 5**
Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka karibu 67 kwa 1,000 (2015/16) hadi takriban 43 kwa 1,000 (2022). Hii inaonyesha maboresho katika chanjo, lishe na matibabu ya magonjwa ya utotoni.

**3. Kongezeka kwa akina mama kujifungulia vituoni**
Idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya imeongezeka kwa kiasi kikubwa, Hii imepunguza hatari za vifo vinavyotokana na kujifungulia nyumbani bila mtaalamu.

KINARA
WA MAONO SEKTA YA AFYA



Swipe Left




**Dkt. Samia ametunukiwa tuzo mbalimbali kwa mafanikio ya Serikali katika kupunguza vifo vya mama na mtoto Tanzania.**

**1. Global Goalkeepers Award – The Gates Foundation (2025)**

Rais Samia alitnukiwa tuzo ya Global Goalkeepers Award iliyotolewa na Bill & Melinda Gates Foundation kutokana na juhudi zake na za serikali yake katika kupunguza vifo vya mama, watoto wachanga na watoto chini ya umri wa miaka mitano, pamoja na kuboresha lishe na huduma za afya kwa familia.

Ni tuzo ya kimataifa inayotambua viongozi waliofanya mabadiliko makubwa kuelekea kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa lengo la afya bora kwa wote, Dkt. Samia aliipokea tuzo hii tarehe Februari 4, 2025 mjini Dar es Salaam, na alikuwa kiongozi wa kwanza kutoka Afrika kukumbukwa kwa heshima



KINARA WA MAONO SEKTA YA AFYA

Swipe Left

Mara baada ya kupokea tuzo hiyo, Rais Samia aliwashukuru wahudumu wa afya nchini kwa mchango wao uliopelekea kupata tuzo hiyo ambayo hutolewa mara moja kwa mwaka kwa watu mashuhuri na viongozi wa kimataifa waliowezesha nchi zao kufanikisha au kuwa na mwelekeo mzuri katika kuyafikia malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka ya Umoja wa Mataifa.

"Wacha nitoe tuzo hii kwa wafanyakazi wote wa afya ambao huruma, ujuzi, na uthabiti wao ulifanya juhudi zetu kuleta mafanikio. Kwa pamoja tunaendelea kutetea malengo ya kimataifa na kuhakikisha kuwa afya inabaki kuwa haki ya wote," amesema Rais Samia.

Mafanikio yaliyopelekea kutolewa kwa tuzo hiyo ni pamoja na ujenzi wa vituo vipya vya afya 183 nchini vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni vimeongezeka na kufikia 523 mwaka 2024 ukilinganisha na vituo 340 vilivyokuwa awali.Tuzo hii ilitambua jinsi uongozi wake umeongeza: huduma za uzazi salama, upatikanaji wa huduma za afya vipatavyo vijijini, uboreshaji wa miundombinu ya afya na utekelezaji wa sera za afya zinazoendana na SDGs.





**2. 'Mother of the Nation Order' – Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)**
Rais Dkt. Samia alitunukiwa nishani ya 'Mother of the Nation Order' na Rais wa Mohamed bin Zayed Al Nahyan ya United Arab Emirates, inayosherehesha uongozi wake wa kuweka ustawi wa jamii na wanawake.

Nishani hii ilitolewa kama kutambua mchango wake katika maendeleo ya jamii na kuimarisha ustawi wa familia, pamoja na ushirikiano na taasisi kama Merck Foundation katika utoaji wa masomo kwa madaktari na kuboresha huduma za afya.

---

**3. 'Utambuzi wa Umoja wa Afrika – AU Champion for Reproductive, Maternal and Child Health (2026)**
Katika kikao cha 39 cha Wakuu wa Nchi na Serikali cha African Union (AU), Rais Samia aliteuliwa rasmi kama AU Champion (Kinara) wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto.

Hii ni nafasi ya heshima inayompandisha kama kiongozi wa ngazi ya Afrika kuongoza juhudi za kuboresha afya ya uzazi na mtoto kwa nchi wanachama wa AU.



**UMOJA WA AFRIKA (AU) wamtangaza Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa KINARA wa Afya ya Mama na Mtoto Afrika**

Umoja wa Afrika (AU) wakati wa kikao cha 39 cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa African Union kilichofanyika Addis Ababa (msimu huu), Rais. Dkt. Samia alichaguliwa rasmi kuwa "AU Champion" kwa afya ya uzazi, mama na mtoto pamoja na haki za afya ya uzazi, Umoja wa Afrika (AU) imemtaja Dkt. Samia Suluhu Hassan kama KINARA wa afya ya mama na mtoto, na hii inamaanisha si tu kwamba anajulikana Tanzania bali pia barani Afrika kwa uongozi wake katika sekta hiyo muhimu.

Umoja wa Afrika inaona afya ya mama na mtoto kama kipengele muhimu kwa maendeleo ya kijamii na uchumi barani Afrika, na kwa kuteua Samia kama kiongozi (champion), inaonyesha kuamini uwezo wake wa kuongoza mpango huo kwa ushirikiano wa nchi za Afrika.

Mhe. Dkt. Samia Anatarajiwa kusukuma sera, mikakati na uwekezaji katika huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa nchi wanachama.



# Rais Dkt. Samia kuzindua Ramani ya utekelezaji ya Kinara wa AU katika afya ya mama na mtoto jijini arusha

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kinara wa Umoja wa Afrika (AU) katika Afya ya Mama na Mtoto, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuzindua rasmi

Ramani ya Utekelezaji ya Kinara wa Umoja wa Afrika katika Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto na Vijana (2026–2030) Tarehe Septemba 9, 2026.

Uzinduzi huo wa kihistoria utafanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), ukiratibiwa sambamba na Kongamano la Pili la Kimataifa la Huduma za Afya ya Msingi linalotajwa kufanyika kuanzia tarehe Septemba 9 hadi 11, 2026.




## Mwelekeo na Shabaha za Ramani ya Utekelezaji (2026–2030)

Ramani hiyo ya miaka mitano inalenga kutoa mwelekeo wa pamoja kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, ikizingatia kubadilisha ahadi na dhamira za kisiasa kuwa hatua madhubuti za kuimarisha mifumo na huduma za afya kote barani. Aidha, mpango huo unalenga:

**Kuongeza Uwajibikaji:**
Kuimarisha usimamizi na ushughulikiaji wa changamoto za afya miongoni mwa nchi wanachama.

**Uwekezaji Endelevu:**
Kuongeza rasilimali na uwekezaji wa kifedha katika sekta ya afya.

**Afua za Kuokoa Maisha:**
Kuharakisha utekelezaji wa afua za haraka zitakazookoa maisha ya wanawake na watoto. Katika ajenda hiyo, msisitizo mkubwa umewekwa kwenye kufikia malengo ya ***"Sifuri Tatu" (Three Zeros)***:



1. Sifuri ya vifo vinavyoweza kuzuilika vya mama na watoto wachanga.

2. Sifuri ya kujifungua katika mazingira yasiyo salama pamoja na rufaa zisizopata huduma stahiki za kitaalamu.

3. Sifuri ya watoto ambao hawajapata chanjo (zero-dose children).

Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, Serikali, jamii, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia na sekta binafsi zinahimizwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mikakati hiyo ili kuboresha huduma za afya kwa makundi hayo muhimu.

## Uteuzi wa Rais Dkt. Samia na Kongamano la Kimataifa

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliteuliwa kuwa Kinara wa Umoja wa Afrika katika Afya ya Mama na Mtoto wakati wa Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Februari 2026.

Kongamano hilo la Kimataifa la Huduma za Afya ya Msingi linatarajiwa kuwakutanisha watunga sera, viongozi wa sekta ya afya, wataalamu, watafiti, washirika wa maendeleo na wabunifu kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika na duniani. Washiriki hao watajadili mikakati ya kuimarisha Huduma za Afya ya Msingi (PHC) na namna ya kuhakikisha huduma bora na zinazopatikana kwa wakati zinafika kwa wananchi wote.

Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania

African Union

AU CHAMPION FOR MATERNAL AND CHILD HEALTH

AfricaCDC
Centres for Disease Control
and Prevention

